# FIDIA eNEWSLETTER




TOLEO LA SITA | APRILI-JULAI 2025 | www.wcf.go.tz

Karibu Sana

WCF
Workers Compensation Fund
ISO 9001 : 2015 CERTIFIED

## YALIYOMO


1. Kupitia WCF, Serikali inawalinda wafanyakazi
2. Fao la Utengamao na Fidia Portal vyazinduliwa katika kilele cha miaka 10 ya WCF
3. Uzinduzi wa mfumo wa kuratibu utekelezaji wa Programu ya Vision Zero (Vision Zero Support System) nchini Tanzania
4. WCF yatumia kipindi cha maadhimisho ya miaka 10 kurejesha kwa jamii
5. Tuzo za WCF


Jarida Mtandaoni Skanii Kodi ya QR Kulia kwako

FIDIA
e NEWSLETTER

ISO 9001 : 2015 CERTIFIED

## TIMU YA WAHARIRI


MWENYEKITI
Dkt. John K. Mduma

MHARIRI MKUU
Laura G. Kunenge

MHARIRI MSAIDIZI
Mcharo S. Mrutu

WACHANGIAJI
Sophia Mtakasimba
Meseka Kadala
Lilian Shembilu

# Dibaji

## Maadhimisho ya Miaka 10 ya WCF

Ni jambo la heshima na fahari kubwa kwangu, kwa niaba ya Menejimenti na wafanyakazi wote wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), kuwakaribisha kwenye jarida hili maalumu linaloangazia safari ya mafanikio ya Mfuko katika kipindi cha miaka 10 cha Uhai wake. Kuanzia mwezi Machi hadi Juni 2025, Mfuko ulitumia kipindi hiki kutekeleza kazi mbalimbali mahususi kama sehemu ya Maadhimisho haya.

Katika kipindi hiki, WCF imekua kwa kasi kubwa na kuwa taasisi ya mfano wa kuigwa katika utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi waliopatwa na madhila kazini. Kupitia dhamira yetu ya kutoa fidia stahiki na kwa wakati, tumeweza kusaidia kurejesha matumaini kwa maelfu ya wafanyakazi na familia zao, huku tukichangia katika kuimarisha ustawi wa rasilimali watu na nguvu kazi nchini.

Mafanikio haya ni matokeo ya juhudi za pamoja za Serikali, watumishi wa WCF, wadau wetu wa ndani na nje ya nchi, waajiri na wafanyakazi wote ambao wamekuwa sehemu ya safari hii. Ushirikiano huu umetuwezesha kuimarisha mifumo yetu ya huduma, kuendeleza matumizi ya teknolojia, na kuhakikisha kuwa sera zetu zinazingatia mahitaji halisi ya jamii ya wafanyakazi.

Tunatambua kuwa bado kuna mengi ya kufanyika na kuboresha. Tunajitazama upya kwa nia ya kuboresha zaidi huduma zetu, kuendelea kujenga uelewa kwa wadau wetu na umma kwa ujumla kuhusu haki na wajibu wa wafanyakazi na waajiri, pamoja na kuimarisha mifumo ya mawasiliano, ufanisi wa utoaji wa fidia, na kushughulikia malalamiko na maoni kwa haraka na kwa haki.

Naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru kwa dhati wadau wetu wote kwa ushirikiano, maoni, na mchango wenu katika kufanikisha kazi ya Mfuko huu. Vilevile, ninawapongeza wafanyakazi wa WCF kwa uaminifu na bidii yao katika kuhudumia wateja wetu na ujenzi wa Taifa letu.

Tukiwa tunaangalia mbele, tunaendelea kujitolea kutoa huduma bora, kwa misingi ya uwazi, weledi na uwajibikaji kwa mustakabali imara wa Mfuko na kwa heshima na ustawi wa kila mfanyakazi wa Tanzania.

Hongereni kwa mchango wenu katika kufikiwa kwa mafanikio haya yaliyopatikana ndani ya miaka 10 ya WCF. Tuendeleze ushirikiano huu katika kipindi cha miaka mingine kumi au zaidi ijayo!

**Dkt. John Mduma**
**Mkurugenzi Mkuu wa WCF**

# "Kupitia WCF, Serikali Inawalinda Wafanyakazi" – Waziri Mkuu Majaliwa



*Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa alizungumza wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 10 ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Julai 04, 2025 jijini Dar es Salaam.*

**Na Mwandishi Wetu**

Serikali kupitia Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) imefanikiwa kutekeleza takwa la kikatiba la kuhakikisha wafanyakazi nchini wanalindwa dhidi ya majanga ya kiuchumi na kijamii yanayotokana na sababu mbalimbali ikiwemo ajali, ulemavu na mgonjwa pamoja na vifo kutokana na kazi kwa kulipa mafao mbalimbali kwa wahanga ikiwemo matibabu, ulemavu wa muda, ulemavu wa kudumu, wategemezi, utengemao, malipo kwa msaidizi wa mgonjwa na gharama za mazishi.

Hayo yamebainishwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa wakati wa Kilele cha Maadhimisho ya Miaka 10 ya WCF yaliyofanyika Julai 04, 2025 jijini Dar es Salaam.

Waziri Mkuu Majaliwa alibainisha kuwa msingi wa kuundwa kwa WCF, pamoja na mambo mengine, unatokana na Ibara ya 11 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inabainisha wazi wajibu wa mamlaka nchini kuhakikisha kwamba zinaweka utaratibu unaofaa wa haki ya mtu katika kufanya kazi, kupata msaada wa jamii wakati wa uzee, maradhi, hali ya ulemavu na katika hali nyinginezo.

"Tangu kuanzishwa kwa WCF mwaka 2015 na kupewa jukumu hili sasa nguvu kazi ya taifa ambayo ni wafanyakazi wana uhakika wa kinga ya kipato pale wanapopata madhila yanayotokana na kazi," alisema Mhe. Waziri Mkuu Majaliwa, na kuongeza kuwa mbali na mafanikio katika kuboresha mafao pia WCF imefanikiwa kufanya kazi kwa uwazi na uwajibikaji kwa kuimarisha mifumo ya TEHAMA, ambapo asilimia 90 ya shughuli za mfuko sasa zinafanywa kidijitali, kupata cheti cha ithibati ya utoaji huduma kwa viwango vya kimataifa pia kurejesha kwa jamii kwa kusaidia sekta ya afya, elimu na mazingira.

Aidha, Mheshimiwa Majaliwa ametoa wito kwa waajiri wote nchini kuhakikisha wanazingatia kikamilifu matakwa ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi ikiwa ni pamoja na

**Inaendelea...**



*Waziri Mkuu akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma kuhusu baadhi ya mafanikio makubwa ya WCF katika kipindi cha miaka 10.*

**Kutoka Ukurasa wa 01**

kujisajili na kuwasilisha michango kwa wakati katika Mfuko, pamoja na kutoa taarifa mapema pale wafanyakazi wanapopata madhila yanayotokana na kazi.

Kwa Upande wake Waziri wa Nchi- Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Ridhiwani Kikwete alisema kuwa katika jitihada za kuendelea kuboresha ustawi wa Wafanyakazi walioumia kazini, Serikali ya Awamu ya Sita imekwishatangaza kwenye Gazeti la Serikali Ongezeko la malipo ya fidia ya kila mwezi kwa wanufaika wa WCF kwa viwango kati ya asilimia 3 hadi asilimia 31 kutegemea na mnufaika alistahili kulipwa kuanzia lini.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma ameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupunguza kiwango cha uchangiaji kwa waajiri wa sekta binafsi kutoka asilimia moja wakati Mfuko unaanzishwa hadi asilimia sifuri nukta tano (0.5%), jambo alilodai kuwa lilikuwa ni kilio cha waajiri cha muda mrefu.

"Tunaipongeza Serikali pia kwa kuwezesha kupunguza kiwango cha riba ya ucheleweshaji wa michango kwa waajiri kutoka asilimia kumi hadi asilimia mbili kwa mwezi. Hatua hii imeongeza imani ya wawekezaji kwa WCF na Serikali kwa ujumla," alisema Dkt. Mduma.

Naye Mwakilishi mkazi wa Kanda ya Afrika Mashariki wa Shirika la Kazi (ILO) Bi. Caroline Mugalla amesema kuwa katika maadhimisho ya miaka 10 ya WCF, jamii inapaswa kukumbuka kuwa kinga ya jamii sio matumizi yasiyo na tija bali ni uwekezaji katika haki, uzalishaji wenye tija unaolifanya Taifa kuwa thabiti. "Tuendelee kujenga Tanzania ambayo kila mfanyakazi anapata huduma stahiki"



*Meza kuu*

# Fao la Utengamao na Fidia Portal vyazinduliwa katika kilele cha miaka 10 ya WCF



*Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa akibonyeza kitufe kuashiria uzinduzi wa Fao la Utengamao wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 10 ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Julai 04, 2025 jijini Dar es Salaam.*

**Na Mwandishi Wetu**

Tukio la Maadhimisho ya Miaka Kumi ya WCF lilienda sambamba na uzinduzi wa Fao jipya la Utengemao linalolenga kumrejesha mfanyakazi aliyepata ulemamavu kwa kumwezesha mfanyakazi aliyeathirika kazini kuendelea na maisha ya uzalishaji, kurejea kazini, kufanya kazi mbadala au kujiajiri, badala ya kubaki kuwa tegemezi pamoja na Lango la Huduma Binafsi la mfanyakazi (WCF Mkononi APP) ambayo inamuwezesha mfanyakazi kuboresha taarifa zake binafsi, kuangalia taarifa za michango yake, kuona na kupakua barua mbalimbali kupitia mfumo, na kufuatilia madai yake ya fidia.



*Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa na meza kuu wakishuhudia maelezo kuhusu namna fao la utengamao linavyofanya kazi.*

# PICHA ZA WADAU NA MATUKIO MBALIMBALI




*Waziri Mkuu na Management ya WCF*




*Waziri Mkuu na Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ya WCF ya sasa na waliowahi kuwa wajumbe*




*Waziri Mkuu na viongozi wa Taasisi Mbalimbali zinazoshughulika na masuala ya kazi*



*Waziri Mkuu na Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini Bw. Abdulaziz Shambe (aliyekaa kwenye kiti mwendo)*



*Baadhi ya Washiriki wakifuatilia*

**Inaendelea...**

Kutoka Ukurasa wa 04












# Uzinduzi wa mfumo wa kuratibu utekelezaji wa Programu ya Vision Zero (Vision Zero Support System) nchini Tanzania



*Prof. Dingani Moyo kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Zimbabwe, akiwasilisha mada kabla ya uzinduzi wa Mwongozo wa 'Vision Zero' uliotafsiriwa kwa Kiswahili.*

**Na Mwandishi Wetu**

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) imetumia maazimisho ya miaka 10 kuzindua mfumo wa kuratibu utekelezaji wa programu ya "Vision Zero" hapa nchini. Program hii inatoa dira katika kutokomeza Ajali, Magonjwa na Vifo kisha kuimarisha Usalama, Afya na Ustawi kwa Wafanyakazi katika Ulimwengu wa kazi. Sambamba na hili umezindua rasmi muongozo uliotafisiriwa kwa Kiswahili ambao ni nyenzo muhimu katika utekelezji wa programu hii.

Uzinduzi huo uliotanguliwa na wasilisho kutoka kwa Prof. Dingani Moyo, Mtaalamu Mbobezi wa masuala ya Usalama na afya kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Zimbabwe, ulihudhuriwa na Wataalamu na wadau wengi katika sekta ya ajira na tasnia ya Usalama na Afya kazini.



*Wadau wa Sekta ya ajira wakiwa wameshika nakala za Mwongozo wa 'Vision Zero' zilizotafsiriwa Kiswahili*

Inaendelea...

Kutoka Ukurasa wa 06

Wadau wakifuatilia uzinduzi wa mfumo wa kuratibu utekelezaji wa Programu ya Vision Zero.










# WCF yatumia kipindi cha Maadhimisho yake ya Miaka 10 kurejesha kwa Jamii



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Ridhiwani Kikwete aakizindua vifaa saidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika Kituo cha Ufundi na Ukarabati kwa Wwatu wenye ulemavu cha Sabasaba mkoani Singida. Anayeshuhudia ni Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, Mkuu wa Mkoa wa Singida Mhe. Halima Dendego*

**Na Mwandishi Wetu**

Katika kuadhimisha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umetoa misaada mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika sekta za afya na elimu pamoja na kuboresha ustawi wa makundi maalum, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa sera yake ya Uwajibikaji wa Kijamii (CSR) kama ishara ya kutambua mchango wa jamii katika mafanikio ya Mfuko huo na kuunga mkono juhudi za Serikali na wadau mbalimbali.

Moja ya maeneo yaliyosaidiwa ni vifaa tiba katika Kituo cha Afya cha Jendele kilichopo Zanzibar, ukarabati wa Kliniki maalum ya madaktari bingwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro ambao umeongeza ufanisi katika utoaji huduma kwa wagonjwa wanaohitaji huduma za kibingwa.

WCF pia ilitoa msaada wa mafuta maalum ya ngozi ya kuzuia mionzi ya jua (sunscreen lotion) na kofia kwa ajili ya jamii ya watu wenye ulemavu wa ngozi. Aidha, Mfuko ulitoa msaada wa viti mwendo, fimbo vyeupe, pamoja na vifaa vya nukta nundu kwa wanafunzi wenye ulemavu katika Kituo cha Ukarabati na Ufundi kwa Watu wenye ulemavu (Sabasaba Vocational and Rehabilitation Center) kilichopo mkoani Singida. Msaada huu umeongeza fursa za ushiriki wa makundi hayo katika shughuli za kijamii na kiuchumi kwa ufanisi zaidi.

Akizungumza wakati wa kukabidhi Kliniki ya Madaktari Bingwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma alisema kuwa dhamira ya WCF ni kujenga jamii jumuishi na yenye ustawi, sambamba na kuadhimisha kwa vitendo mafanikio ya Mfuko katika kipindi cha Miaka Kumi.

**Inaendelea...**




Baadhi ya vifaa vilivyokabidhiwa

"Kupitia shughuli hizi, Mfuko umedhihirisha kuwa mafanikio ya miaka 10 si tu kwa kutoa fidia kwa wafanyakazi, bali pia katika kuchangia ustawi na maendeleo ya kijamii na kuboresha maisha ya wananchi," alisema Dkt. Mduma.



*Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma akipokea cheti cha shukrani kutoka kwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Dkt. Best Magoma kutokana na kutambua mchango wa Mfuko huo katika kuboresha huduma za afya katika hospitali hiyo.*




*Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi Bi. Veronica Saeni, akikabidhi kwa Mganga Mkuu Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Zanzibar, Dkt. Amina Hussein Pandu vifaa tiba kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma za afya katika Kituo cha Afya Jendele, Zanzibar.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Bi. Laura Kunenge(wa kwanza kulia) akiwa kwenye picha ya pamoja na Viongozi wa Chama ya Watu wenye Ualbino (TAS) mara baada ya kukabidhi msaada wa kofia na mafuta ya kuthibiti mionzi ya jua (Sunscreen) Mjini Kigoma, wakati wa kilele cha maadhimisho ya siku ya kuongeza uelewa kuhusu ualbino.*

# WCF Yatoa Tuzo kwa Wadau Kutambua Mchango Wao Katika Maadhimisho ya Miaka 10

**Na Mwandishi Wetu**

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umetunuku tuzo kwa wadau mbalimbali ikiwa ni sehemu ya kilele cha maadhimisho ya miaka 10 tangu kuanzishwa kwake, kama ishara ya kutambua mchango wa wadau hao katika kuboresha mazingira ya kazi, usalama kazini na utoaji wa huduma kwa wafanyakazi waliopatwa na madhira wakiwa kazini.

Sherehe hizo, zilizofanyika jijini Dar es Salaam, zilibeba kaulimbiu ya "Miaka 10 ya Fidia kwa wafanyakazi: Kazi iendelee kuhudhuriwa na viongozi wa serikali, wawakilishi wa sekta binafsi na za kiraia, waajiri, wanufaika wa WCF na washirika mbalimbali wa maendeleo.

## Tuzo Maalum ya Shukran

Katika kutambua mchango wa viongozi walioweka msingi wa WCF, tuzo maalum za shukrani zilitolewa kwa:



•CPA Masha Mshomba – Mkurugenzi Mkuu mwanzilishi wa WCF, ambaye alihusika kikamilifu katika uanzishwaji wa Mfuko na kusimamia hatua za awali za ujenzi wa mifumo ya huduma kwa wafanyakazi.



•Mr. Emmanuel Humba – Mwenyekiti wa kwanza wa Bodi ya Wadhamini ya WCF, ambaye aliongoza bodi katika kipindi muhimu cha mwanzo wa uendeshaji wa Mfuko

## Tuzo kwa Waajiri na Wanufaika wa Mfuko

Katika kutambua ushiriki wa waajiri na wanufaika katika mafanikio ya WCF, tuzo zifuatazo zilitolewa:



•Mwajiri wa kwanza kuchangia Mfuko: STRABAG International – Kampuni ya kwanza kutoa mchango rasmi kwa WCF mara baada ya kuanzishwa kwake mwaka 2015.



•Mwajiri mkubwa anayechangia kwa wakati na kuwasilisha taarifa kwa usahihi: NMB Bank Public Limited Company

Inaendelea...

Kutoka Ukurasa wa 10

# WCF Yatoa Tuzo kwa Wadau Kutambua Mchango Wao Katika Maadhimisho ya Miaka 10



•Mwajiri kutoka asasi za kiraia anayechangia kwa wakati na kwa usahihi: Tanzania Health Promotion Support (THPS)



•Waajiri wanaotumia vyema mfumo wa WCF–Online Notification System:
oTPC Ltd




•Mnufaika wa kwanza wa huduma za WCF. Masoud Mkumbukwa – aliyepata fidia ya kwanza kutoka kwa Mfuko.



oLodhia Industries Ltd



•Mwajiri anayetumia vizuri mfumo wa kutoa taarifa za ajali na kuboresha afya na usalama kazini: A TO Z Group Ltd



•Waajiri waliowekeza katika mifumo na teknolojia ya kuzuia ajali kazini:
oGeita Gold Mining

Inaendelea...

Kutoka Ukurasa wa 11

# WCF Yatoa Tuzo kwa Wadau Kutambua Mchango Wao Katika Maadhimisho ya Miaka 10



oBulyanhulu Gold Mine

## Tuzo kwa Watoa Huduma za Afya

Kwa upande wa sekta ya afya, hospitali mbalimbali zilipokea tuzo kutokana na mchango wao katika kuwahudumia wanufaika wa WCF kwa ubora, weledi na kwa wakati. Zifuatazo ni hospitali zilizotunukiwa:



•Hospitali inayohudumia wanufaika wengi wa WCF: MOI (Muhimbili Orthopaedic Institute)



•Hospitali inayojaza Medical Forms za WCF kwa usahihi: JKCI – Dar Group



•Hospitali zinazotoa huduma za utengemao kwa wanufaika wengi:
oCCBRT



oKCMC



•Hospitali ya rufaa ya kanda inayohudumia wateja wengi wa WCF: Mbeya Zonal Referral Hospital

Kutoka Ukurasa wa 12

# WCF Yatoa Tuzo kwa Wadau Kutambua Mchango Wao Katika Maadhimisho ya Miaka 10



•Hospitali binafsi inayohudumia wateja wengi wa WCF: Arusha Lutheran Medical Centre (ALMC)



•Hospitali inayozingatia muda katika kuwahudumia wanufaika: Morogoro Regional Referral Hospital

## TAARIFA YA KUHAMA KWA OFISI

**Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, (WCF)** unapenda kuwafahamisha kuwa Ofisi zake zilizokuwa ghorofa ya 6, jengo la Victoria house, barabara ya Bagamoyo, sasa zimehamia **ghorofa ya 7**, jengo la **Commercial Tower**, Barabara ya **Sam Nujoma.**

**KARIBU TUKUHUDUMIE**

Imetolewa na
Kitengo cha Uhusiano kwa Umma
Simu namba 0800 11 00 28 | 29

ISO 9001 : 2015 CERTIFIED

Jarida hili limeandaliwa na
Kitengo cha Uhusiano kwa Umma WCF:
MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI (WCF)
Jengo la Kambarage, Ghorofa ya 3,
S.L.P 329, 41104 Dodoma,
TANZANIA